

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA

18 MEI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA – TAREHE 18 MEI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

360. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA (SEGEREA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Bima hadi Mawenzi – Kimanga kwa kiwango cha lami.

361. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, ni sahihi kwa Watendaji kuwazuia Wabunge kukagua Miradi ya Maendeleo na kuwanyima taarifa za utekelezaji katika Majimbo yao.

362. MHESHIMIWA MARIAM MADALU NYOKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaweka utaratibu rahisi wa Mikopo kwa Wakulima Wadogo hasa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Ruvuma.

363. MHESHIMIWA ENG. JOHNSTON JOHANSEN MUTASINGWA (BUKOBA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea Vijana waendesha Pikipiki maeneo ya maegesho.

364. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukarabati Zahanati ya Kijiji cha Kalemawe kwa kuwa ni chakavu.

WIZARA YA UJENZI:

365. MHESHIMIWA ADO SHAIBU ADO (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya lami kutoka Nachingwea hadi Tunduru kupitia Vijiji vya Napa na Mindu utaanza na kukamilika.

WIZARA YA KILIMO:

366. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Skimu nne za Umwagiliaji katika Bonde la Umba kama ilivyoahidi.

367. MHESHIMIWA YAGI MAULID KIARATU (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji katika Jimbo la Singida Mjini ili kuongeza uzalishaji wa kilimo.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

368. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itaanzisha Minada ya Kimataifa ya Mifugo katika Jimbo la Tarime Vijijini.

WIZARA YA MAJI:

369. MHESHIMIWA ENOCK ZADOCK KOOLA (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kwa nini MUWASA na RUWASA wasichimbe visima virefu na mabwawa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri Wananchi wa Vunjo.

**370. MHESHIMIWA ENG. CHACHA MWITA WAMBURA
(GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha Miradi ya Maji Kata za Bulela, Shiloleli, Bung'wangoko, Nyanguku na Ihanamilo Geita Mjini.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**371. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO
(TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Wilaya ya Tarime itapata Gari la Zimamoto la kisasa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
18 MEI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**